



## **BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

### **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

### **BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI**

### **MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 20 Februari, 2018.**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua itasomwa.

#### **I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

##### **Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2017/2018.

#### **II. MASWALI:**

##### **Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:**

38. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kwa kuwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kisheria inasimamia na kuzitunza mali zote zilizo chini ya kamisheni hiyo, jambo ambalo linasaidia kupatikana kwa haki kama ilivyotarajiwa. Na kwa kuwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina mashamba ya aina tofauti kama vile mashamba ya minazi, mikarafuu n.k.

- (a) Je, kwa sasa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina mashamba mangapi ambayo yalitolewa wakfu wa Misikiti.
- (b) Je, shamba la Baziadi iliyopo Bwagamoyo Mtambwe ilitolewa Wakfu kwa ajili ya kushughulikia misikiti mingapi.
- (c) Je, kuna utaratibu gani uliopangwa wa kupanda miti mengine mashamba yote ya Wakfu ambayo kwa sasa inaonekana kwamba miti ya asili iliyokuwemo kwa wakati huo imeshakuwa mikongwe.

**Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:**

72. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHANI SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetunga sheria kali katika kupambana na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Hata hivyo, yapo mambo yanayosababisha kuendelea kwa udhalilishaji kama watoto kuachiliwa kutembea usiku na wanawake kutovaa mavazi ya heshima.

- (a) Je, suala la watoto kutembea usiku bila kikomo na suala la wanawake kutembea na mavazi yasiyokuwa na heshima hayachangii udhalilishaji huo.
- (b) Kama hauchangii miaka ya nyuma iliyopita kulikuwa na kikomo cha muda wa kutembea usiku na wanawake kuvaa nguo za heshima, je kulikuwa na sababu zipi za kufanya hayo.
- (c) Pamoja na juhudi zote za Serikali, bado suala hili kama limetiwa mafuta ya petroli na moto, Je, Serikali imeona nini sababu zake.

**Wizara ya Afya:**

48. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na habari njema za kupatikana kwa “mortuary freezer” katika hospitali ya Mnazi Mmoja jambo ambalo litasaidia sana kuhifadhi maiti na ni faraja kubwa kutokana na kuwa tulikuwa na tatizo hilo.

- (a) Je, kifaa hicho kina uwezo wa kuhifadhi maiti wangapi kwa wakati mmoja.
- (b) Je, thamani ya kifaa hicho ni kiasi gani.
- (c) Je, “mortuary freezer” hiyo ni msaada kutoka wapi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**

59. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) -  
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi,  
Mawasiliano na Usafirishaji:

Katika Shehia ya Sizini Kijichame, Mitungujani na Ziwatuwe kumejitokeza tatizo la mawasiliano kupitia mtandao wa Zantel kwa kipindi cha miezi minne (4) sasa.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuibuka kwa tatizo hilo ambalo huko nyuma halikuwepo.

**III. HOJA ZA KAMATI:**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2017/2018.

Zanzibar,  
20 Februari, 2018.

(Raya Issa Msellem)  
KATIBU WA BARAZA.